**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia uhai na uzima na tukaweza kufika hapa leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu na tukaweza kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu anijaalie nguvu na ufasaha niweze kuwasilisha Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili tuweze kuichangia kwa umakini na hatimae kuipitisha bajeti ya Wizara hii kwa maslahi ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza Nchi hii, pamoja na jitihada anazozichukua za kimapinduzi ya kiuchumi katika kuhakikisha analeta

maendeleo na mabadiliko ya kasi katika Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, napenda kuchua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awazidishie busara pamoja na hekima katika kutekeleza majukumu yenu ya kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika Chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

**Vile vile,** nichukuwe fursa hii kumpongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Mhe. Tabia Maulid Mwita pamoja na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Fatma Hamad Rajab, Afisa Mdhamini Pemba Ndg. Mfamau Lali Mfamau, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote kwa mashirikiano yao waliyotupatia wakati wa kutekeleza majukumu yetu ya kamati ya kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na kupata ufumbuzi wa masuala mbali mbali..

**Mheshimiwa Spika,** Kiupekee kabisa Nachukuwa Fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa kamati yangu kwa mashirikiano na umoja wao kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa kupitia bajeti ya wizara hii kwa ufanisi mkubwa kwani tulikuwa bega kwa bega na Waheshimiwa Wajumbe hawa wakati wa kuyajadili makadirio na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zitakazoingizwa kwa wizara hii zinakwenda kutumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali (Jazeera) | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Choum Kombo Khamis | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| 11. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu. |

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ina mafungu mawili (2) ambayo ni Fungu J03 na Fungu J05. Kwa upande wa fungu J03 lina program kuu nne (4) na program ndogo nane (8) ambazo zinakadiriwa kutumia shilingi bilioni 453,391,093,000/- na fungu J05 lina program kuu mbili (2) na program ndogo tatu (3) ambazo zinakadiriwa kutumia shilingi bilioni 1,456,900,000/- hivyo jumla ya fedha zilizoombwa kwa wizara ya Habari Vijana, Utamaduni na Michezo ni shilingi bilioni 454,847,993,000/- na shilingi 633,982,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara kutoka Tzsh. Bilioni 89.2 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi

kufikia Tzsh. Biloni 453.3 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati imeelezwa kuwa ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo hasa katika uimarishaji wa michezo na miundombinu ya viwanja vya michezo ikiwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali katika Wizara hii.

## FUNGU J03

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii inatekelezwa chini ya Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni SJ030101 Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na SJ030102 Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji, ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu Kuu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 9,167,152,000/= ambapo makadirio yake yamepungua ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2024/2025 ambayo yalikua Tzsh. Bilioni 10.3

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuiangalia kwa undani zaidi Bajeti ya programu hii kwa sababu uendeshaji wake unahitaji fedha za kutosha na programu hii haina mapato inayoyategemea isipokuwa uuzaji wa picha za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa msimu hasa kwa Idara ya Habari Maelezo pamoja na kutoa liseni kwa Vyombo vya Habari ukizingatia kipindi hiki cha tunachoekea katika Uchaguzi Mkuu wa nchi, Vyombo vya Habari vinataka usimamizi wa hali ya juu ili kuepuka kutoa habari za uchochezi katika nchi yetu na kuendelea kuwa na amani katika kipindi chote cha uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali Kupitia wizara kwa ujenzi wa kiwanda cha Magazeti pamoja na nyumba za wafanyakazi katika mradi unaoendelea kutekelezwa Tunguu. Kiwanda hicho kitakwenda kupunguza gharama kubwa kwa Shirika kwenda kuchapisha magazeti Tanzania Bara. **Pia,** Kamati inashauri wizara mbali na ujenzi huo kuharakisha ununuzi wa mtambo mpya wa kisasa wa kuchapisha magazeti utakaowezesha kufanya kazi hii wa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inalipongeza Shirika la Utangazaji ZBC kwa kuwa na makusanyo mazuri yaliyovuka kiwango katika mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha kamati imeona ipo haja kwa wizara kuifanyia marekebisho Sheria ya Habari ya Mwaka 1997 ili iweze kwenda sambamba na wakati tulionao na kupelekea kukushanya mapato mengi zaidi.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA (PJ0302)

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii PJ0302 ina program ndogo moja (1) ya Maendeleo ya vijana (SJ030201), Bajeti ya programu hii imeongezeka kutoka Tsh. bil 5,662,714,000 kwa mwaka 2024/2025 hadi kufikia Tsh. Bil 18,260,503,000 kwa mwaka 2025/2026. Hata hivyo, kamati inasisitiza Wizara husika kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa wakati kwa vile katika mwaka wa Fedha 2024/2025 ni aslimia 3 tu ya fedha za Mradi wa Maendeleo ya vijana zilizopatikana.

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kusimamia vizuri ujenzi wa miradi ya maendeleo ya Vijana sambamba na kuyasimamia mabaraza ya vijana yaweze kujiendesha na kujikwamua kiuchumi. vile vile ipo haja kwa Serikali kupitia Tume ya Mipango kuliangalia Zaidi fungu hili la vijana

katika miradi ya vipaumbele ili kwenda sambasamba na Sera ya Serikali katika kuwaendeleza vijana.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO (PJ0303).

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni imarishaji, uhifadhi na uendelezaji wa utamaduni, Sanaa na ubunifu (SJ030301) na Uimarishaji wa michezo na miundommbuni ya viwanja vya michezo (SJ030302)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono jitihada za Serikali za kuendeleza Michezo nchini ambapo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 fungu la Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo limepanda kutoka Bil 69.2 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi kufikia Bil 421.8. Kamati ilihoji juu ya engezeko kubwa la Fedha katika Program hii na kuarifiwa kwamba Serikali imetenga eneo kubwa kwa ajili ya ujenzi wa SPORT CITY katika eneo la Fumba Town ambalo litatumika katika michezo ya Afcon 2027 Ambapo Wizara inatarajia kujenga Kiwanja kikubwa cha kisasa kitakachokidhi vigezo vya kimataifa Sambamba na viwanja vyengine kwa ajili ya mazoezi na shughuli za kitaifa pamoja na Hospital, Bandari, Hoteli na Kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kuendelea kutekeleza miradi mbali mbali katika Wizara hii ikiwemo ujenzi wa viwanja vya michezo pamoja na nyumba ya Sanaa,
Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuwashirikisha wataalamu husika tokea mwanzoni mwa miradi ili kuepusha gharama za ziada ambazo

hujitokeza kutokana na kukosekana kwa mahitaji muhimu katika miradi mingi ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Uimarishaji, uhifadhi na uendelezaji wa sekta ya utamaduni, sanaa na ubunifu ni suala muhimu katika jamii au Taifa. Kamati inaikumbusha Serikali kulipa kipaumbele suala hili kwa vile utamaduni ni kielelezo muhimu na utambulisho katika maendeleo ya nchi hivyo ipo haja kwa serikali kuzingatia Bajeti yake katika kuona Utamaduni wa Mzanzibar unakua, unatambulika na kuimarika.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI (PJ0304).

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo tatu (3); Mipango, Sera na Utafiti **(SJ030401)**, Utumishi na Uendeshaji (**SJ030402)** na Uratibu wa shughuli za wizara Afisi kuu Pemba **(SJ030403).** Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji imekadiriwa kutumia shilingi Bilioni 4,129,582,000/= kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuingizia fedha za miradi kwa wakati na kuepusha usumbufu kwa Wizara husika kwani wanatumia fedha za O.C ili miradi iweze kutekelezeka na baadhi ya shughuli nyengine kuchelewa kufanyika ikiwemo shughuli za ndani za Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuwaendeleza watendaji wake kwa masomo ya muda mrefu na muda mfupi hasa katika masuala ya teknolojia ya Habari ili waendane na wakati uliopo.

## FUNGU J05 TUME YA UTANGAZAJI.
## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI NA UTANGAZAJI (PJ0501)

**Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii inatekelezwa chini ya Programu Ndogo moja usimamizi wa vyombo vya utangazaji (SJ**050101),** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi milioni 172,018,000/=.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za fungu hili kutoka shilingi milioni 284.1 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 hadi shilingi milioni 172 kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwani usimamizi wa Vyombo vya Habari pamoja na Utangazaji vinahitaji fedha nyingi za kuweza kuendesha shughuli zao.

Kamati inashauri Serikali kuipatia ruzuku Tume ya Utangazaji ili iweze kukidhi mahitaji ya kazi zao ambazo wanakwenda kuzitekeleza pia ipo haja kwa Wizara kuifanyia marekebisho Sheria Nam.7 ya Utangazaji ya Mwaka 1997 ili iweze kwenda sambamba na wakati uliopo wa Sayansi na Technolojia.

Kamati inashauri Serikali kuipatia jengo la kudumu Tume ya Utangazaji sambamba na vifaa vya kutosha pamoja na miundombinu ya kisasa ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuendeleza mashirikiano na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ambayo imekuwa na wigo mpana katika utekelezaji wa kazi zake katika sekta ya utangazji na mawasiliano nchini.

## PROGRAMU KUU YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika,** Program kuu hii PJ0502 inatekelezwa chini ya program ndogo mbili (2) ambazo ni utumishi (SJ050201) na uwendeshaji (SJ050202). Jumla ya shilingi bilioni 1,284,882,000/- zimepangwa kutumika katika Programu hii kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026.

Kamati, inaipongeza Serikali kwa kuona ipo haja kuliongezea bajeti fungu hili kutoka shilingi Bilioni 1,200,029,000 hadi kufikia shilingi 1,284,882,000 ili wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara husika kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuwapatia kibali cha uwajiri tume ya utangazaji ili kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi sambamba na kuwajengea uwezo watendaji wake kwa masomo ya muda mrefu na muda mfupi hasa katika masuala ya teknolojia ya Habari ili waendane na wakati uliopo.

## HITIMISHO,

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kwa vile Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa

mwaka wa fedha 2025/2026, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha ujao.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

…………………………………………

Mhe, Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

**ZANZIBAR.**